# HOJA YA ISLAM

na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

# HOJA YA ISLAM

Tafsiri ya Kiswahili ya: *Hujjatul-Islam* (Urdu)

Na: Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

Mfasiri: Sheikh Bakri Abedi Kaluta

© Islam International Publications Ltd.
Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1900
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2019

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
S.L.P. 376, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 978 1 84880 543 9
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ [1]

نَحْمَدُهٗ وَ نُصَلِّي عَلٰى رَسُولِهِ الْكَرِيمِ [2]

# MAELEZO YA MWENEZI

## KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as], alizaliwa tarehe 13 Februari 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alijitolea kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi ya maana sana ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. (Mwenezi)

[2] Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu. (Mwenezi)

na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam Mahdi na Masihi Mau'udi, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume[saw]. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 197 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha mpango wa Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba].

**KUHUSU KITABU**

Naona furaha kuweka mbele ya wasomaji tafsiri hii ya kitabu cha Seyyidna Ahmad[as], Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, kiitwacho "*Ḥujjatul-Islām*" (Hoja ya Islam) kilichochapishwa mnamo 8 Mei 1893, ambamo Dr. H. Martyn Clark na baadhi ya Wakristo wameitwa kwenye dai hili lenye shani kwamba Islam pekee ndiyo dini iliyo hai na yenye baraka na nuru ya kimbingu ndani yake, ambayo hadi sasa inazo ishara za uthibitisho wake kama ilivyokuwa nazo hapo awali. Na pia imeelezwa hivi ndani ya kijitabu hiki

kwamba dini ya Kikristo imo ndani ya kiza na kwamba ndani yake hamna alama za dini iliyo hai. Na pia ule mjadala uliopangwa tarehe 22 Mei 1893, yametajwa humu masharti yake yaliyo muhimu pamoja na matangazo mengine yanayohusiana na Sheikh Muhammad Husein wa Batala.

# SHUKRANI

Kitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na Sheikh Bakri Abedi Kaluta, Mbashiri wa Tanzania.


Hapa Makao Makuu katika Deski ya Kiswahili Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania na Kenya na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri wa zamani wa Tanzania, Kenya na Ghana waliichunguza tafsiri hii kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana na kuidurusu.

Aidha ndugu kadhaa wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Sharifu Tanwir Mujtaba na Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na Akubali huduma yao. Amin.

Chaudhry Muhammad Ali M.A.
Wakilut-Tasnif
Tahrik-e-Jadid
Rabwah. Pakistan
1 Agosti, 2015

(PICHA YA UKURASA WA KWANZA WA NJE)



ٹائیٹل بار اوّل

الحمد للہ والمنۃ کہ رسالہ تالیف کردہ مجدد دوران
مسیح الزمان مرزا غلام احمد رئیس قادیان
موسوم بہ

# حُجَّۃُ الاِسْلَام

جسمیں ڈاکٹر ایچ مارٹن کلارک صاحب اور بعض دوسرے
عیسائی صاحبوں کو اس عظیم الشان دعوت کے لئے بلایا گیا ہے کہ دنیا
میں زندہ اور بابرکت اور آسمانی روشنی اپنے اندر رکھنے والا مذہب صرف
اسلام ہی ہے جس کے ثبوت کے نشان اب بھی اُسکے ساتھ ایسے ہی ہیں
جیسا کہ پہلے تھے اور اس رسالہ میں یہ بھی بیان کیا گیا ہے کہ عیسائی مذہب
تاریکی میں پڑا ہوا ہے اور زندہ مذہب کی علامتیں اس میں موجود نہیں ہیں اور
جو ۲۲ مئی ۱۸۹۳ء کو مباحثہ قرار پایا ہے اسکی ضروری شرائط بھی اسمیں درج
ہو کر معہ بعض اور اشتہارات کے جو شیخ محمد حسین بٹالوی وغیرہ کے متعلق ہیں

اتمام حجت کی غرض سے ۸ مئی ۱۸۹۳ء کو باہتمام شیخ نور احمد صاحب
مہتمم مطبع ریاض ہند امرتسر میں شائع ہوا

تعداد جلد ۷۰۰ — قیمت فی جلد ۱ر

(TAFSIRI YA UKURASA WA KWANZA WA NJE)

Sifa zote njema na hisani ni za Mwenyezi Mungu kwamba kijitabu kilichoandikwa na Mujaddidi wa zama hizi na Masihi wa zama hizi, Mirza Ghulam Ahmad, chifu wa Qadian, kiitwacho

# Hujjatul Islam

ambamo Dr. H. Martyn Clark na baadhi ya Wakristo wengine wametolewa mwito huu wenye shani kubwa kwamba Islam pekee ndiyo dini iliyo hai na yenye baraka na nuru ya kimbingu ndani yake, ambayo hata sasa inazo ishara za uthibitisho wake kama zilivyokuwa hapo awali. Na imeelezwa pia ndani ya kijitabu hiki kwamba dini ya Kikristo imo kizani na ndani yake hamna alama za dini iliyo hai. Na ule mjadala uliopangwa kufanyika tarehe 22 Mei 1893, masharti yake ya muhimu pia yametajwa humu pamoja na matangazo mengine yanayohusiana na Sheikh Muhammad Husein wa Batala na wengineo.

Kimechapishwa tarehe 8 Mei 1893 ili kutimiza hoja,
chini ya usimamizi wa sheikh Nur Ahmad,
msimamizi wa kiwanda cha uchapaji Riyadh Hind,
Amritsar

Bei ya kila nakala: 1 ana Nakala: 700

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكّٰىهَا ۝[3]

*Yeyote ampendaye Yule Mtakatifu,*
*kwanza ajitakase ndipo atakapompata Yeye.*

Hili ni dai la kila kaumu kwamba wengi miongoni mwetu ndio wampendao Mwenyezi Mungu, lakini uthibitisho unaotakiwa ni huu kwamba je Mungu Naye Anawapenda au la? Na mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni haya kwamba kwanza Awaondolee pazia mioyoni mwao ambayo kwa sababu ya pazia hiyo mwanadamu huwa hana yakini barabara ya uwepo wa Mwenyezi Mungu, na anaamini uwepo Wake kwa utambuzi kidogo wenye giza-giza. Bali mara nyingi wakati wa mtihani, huukataa hata uwepo Wake. Na kuondolewa kwa pazia hii hakuwezekani kwa njia nyingine yoyote isipokuwa kwa maongezi na Mungu. Basi mwanadamu anapiga mbizi ndani ya chemchemi ya utambuzi wa kweli wa Mwenyezi Mungu siku ambayo Mwenyezi Mungu Humpa bishara ya kumwambia '*Anal Maujuud*' (yaani Mimi Nipo). Hapo maarifa ya mwanadamu yanakuwa hayaishii tu kwenye makisio ya dhana zake au kwenye mawazo yanayotegemea maandiko, bali husogea karibu na Mwenyezi Mungu kana kwamba anamwona. Na hii ni kweli na ni kweli tupu kwamba

[3] Bila shaka amefaulu aliyeitakasa. Ash-Shams, 91:10. (Mwenezi)

mwanadamu hujaliwa imani kamili juu ya Mwenyezi Mungu siku ile tu Mwenyezi Mungu Anapompasha Mwenyewe habari ya uwepo Wake. Halafu alama ya pili ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu ni hii kwamba sio tu Anawapa waja Wake wapenzi habari ya uwepo Wake, bali Huwadhihirishia pia athari hasa za rehema na fadhili Zake, nayo ni hivi kwamba Akizikubali dua zao zaidi kuliko matarajio yao Huwapasha habari kwa njia ya ufunuo na maneno Yake, hapo mioyo yao hupata utulivu kwamba Huyu ni Mungu wetu Mweza ambaye Huyasikia maombi yetu na kutupasha habari na kutuokoa toka kwenye matatizo. Ni siku hiyo hiyo suala la wokovu pia huja kufahamika na pia uwepo wa Mwenyezi Mungu huja kutambulika. Ingawa wakati mwingine hata watu wengine huweza kujiwa na ndoto za kweli ili kuwazindua na kutanabahisha, lakini daraja na shani na hali ya njia hii ni tofauti. Hayo ni maongezi ya Mwenyezi Mungu ambayo huwa ni makhsus kwa ajili ya waliokurubishwa kwake. Na wakati mwanadamu aliyekaribishwa kwa Mwenyezi Mungu aombapo dua, basi Mwenyezi Mungu, pamoja na ujalali Wake wa kiungu Humdhihirikia na kumteremshia roho Yake na Humpa bishara za kukubalika kwa maombi yake kwa maneno Yake yaliyojaa upendo. Na yule ambaye hufanyiwa maongezi haya kwa wingi huitwa nabii au muhaddath. Na hii ndiyo alama ya dini ya kweli kwamba kutokana na mafundisho ya dini

hiyo waendelee kupatikana watawa wenye kufikia hadi daraja la Muhaddath ambao Mwenyezi Mungu huongee nao ana kwa ana. Na alama ya kwanza ya ukweli na uhakika wa Islam ni hii hii kwamba daima hupatikana humo watawa ambao Mwenyezi Mungu Huongea nao.

تَتَنَزَّلُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُواْ وَلَا تَحۡزَنُواْ [4]

Basi hiki ndicho kipimo cha dini ya haki, ya ukweli, yenye uhai na yenye kukubalika. Nasi twafahamu kwamba nuru hii imo ndani ya Islam tu, dini ya Kikristo haikubahatika na nuru hii. Na hoja yetu hii iliyo kwa Dr. Clark ndiyo kwa kusudio hili na sharti hili hili kwamba kama yeye ayakatae mashindano haya, basi mfahamu kwa yakini kwamba dalili hii hii moja ni zaidi ya dalili elfu katika kuibatilisha dini ya Kikristo kwamba kamwe mfu hawezi kushindana na aliye hai wala kipofu hawezi kukabiliana na mwenye kuona.

*Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo*

5 Mei 1893

Ni mimi Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian, Wilaya la Gurdaspur.

---

[4]Huwateremkia Malaika wakiwaambia msihofu wala msihuzunike. Haa Miim, 41:31. (Mwenezi)

بِسْم اللّٰه الرّحمٰن الرّحيم [5]

نَحْمَدهٗ وَ نُصَلِّی علٰی رسولهِ الکَرِیُم [6]

# VITA VITAKATIFU VYA DAKTARI PADRI CLARK NA TANGAZO LA KUPAMBANA NAYE

Iwe wazi kwamba bwana Daktari aliyetajwa juu amedhihirisha katika baadhi ya barua zake tashi hili kwamba anajitayarisha kwa vita vitakatifu dhidi ya wanazuoni wa Kiislamu. Pia amedhihirisha ndani ya barua yake kwamba vita hivi vitafanyika kwa kusudio la kupata uamuzi kamili. Na pia akatoa tishio hili kwamba kama wanazuoni wa Kiislamu wakiukwepa vita hivi au wakishindwa vibaya, basi hawatakuwa na haki katika siku zijazo ya kuweza kusimama ili kukabiliana na wanazuoni wa Kikristo au ya kuweza kuifahamu dini yao kuwa ni ya kweli au ya kuweza kusema lolote mbele ya Wakristo. Kwa kuwa mimi nimetumwa kuja kupigana nao vita hizi hizi za kiroho, na pia ninafahamu kwa kupata ufunuo toka kwa Mwenyezi Mungu kwamba katika kila uwanja ushindi ni wetu, hivyo mara moja bwana Daktari amefahamishwa kwa njia ya barua kwamba ni utashi wetu hasa kwamba vita hivi vifanyike ili ukweli na uwongo

[5] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. (Mwenezi)

[6] Tunamhimidia yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu. (Mwenezi)

upambanuke kwa uwazi kabisa. Na haikuishia hapa, bali marafiki wachache wenye kuheshimika wakiwa wajumbe wa mwito wa 'vita' walitumwa Amritsar kwa bwana Daktari ambao majina yao mashuhuri ni haya:

1. Bwana Mirza Khudaa Bakhsh
2. Bwana Munshi Abdul Haq
3. Bwana Hafidh Muhammad Yusuf
4. Bwana Sheikh Rahmatullah
5. Bwana Maulawii Abdul Karim
6. Bwana Munshi Ghulam Qaadir Faswiih
7. Bwana Mian Muhammad Yusuf Khan
8. Bwana Sheikh Nur Ahmad
9. Bwana Mian Muhammad Akbar
10. Bwana Hakim Muhammad Ashraf
11. Bwana Hakim Ni'matullah
12. Bwana Maulawii Ghulam Ahmad, Mhandisi
13. Bwana Mian Muhammad Bakhsh
14. Bwana Khalifa Nuruddin
15. Bwana Mian Muhammad Ismail

Ndipo kukafanyika mazungumzo kati ya Bwana Daktari na wale marafiki zangu walioniwakilisha na kuafikiana

jambo hili kwamba mjadala huu ufanyikie huko Amritsar. Na kwa upande wa Padri akapendekezwa mzungumzaji wa mjadala huu Bwana Abdullah Atham, Extra Assistant wa zamani. Na hii pia ikapendekezwa na upande wao kwamba pande zote mbili zitakuwa na ruhusa ya kuwa na wasaidizi watatu. Na kila upande utapewa siku sita za kuukosoa upande wa upinzani, hivi kwamba kwa siku sita za mwanzo itakuwa ni haki yetu kukosoa dini, mafundisho na itikadi za upande wa upinzani. Kwa mfano tuombe uthibitisho wa uungu wa Hadhrat Masihi na kuwa kwake mwokozi au tutoe hoja lingine lolote linaloweza kutolewa dhidi ya dini ya Kikristo. Halikadhalika upande wa pili pia utakuwa na haki ya kwamba kwa siku sita waendelee kuyakosoa mafundisho ya Kiislamu. Na hii pia ikakubaliwa kwamba kwa ajili ya kukidhibiti kikao hicho ateuliwe mwenyekiti wa kikao toka kila upande atakayelizuia kundi la upande wa upinzani lisifanye fujo, vitendo visivyostahili na kuingilia kati mjadala. Na jambo hili pia likakubaliwa kwa pamoja na kuafikiwa kwamba kila upande hautakuwa na zaidi ya watu hamsini, na pande mbili zichapishe tiketi mia moja ambapo kila upande ugawe tiketi hamsini kwa watu wake na hakuna yeyote atakayeweza kuingia ndani bila ya kuonyesha tiketi. Na hatimaye, kutokana na ombi makhsus la bwana Daktari, ikakubaliwa kwamba mjadala huu unapaswa kuanza mnamo tarehe 22 Mei 1893.

Maandalizi ya eneo la mjadala na uteuzi wa eneo la mjadala uliachwa mikononi mwa bwana Daktari na yeye ndiye atakayekuwa mwajibikaji wake. Na baada ya kuafikiana taratibu zote hizi bwana Daktari na ndugu yangu bwana Maulawii Abdul Karim wakatia saini kwenye maandiko haya ambamo masharti hayo yaliandikwa kwa kirefu na ikakubaliwa kwamba hadi tarehe 15 Mei 1893 pande mbili ziwe zimechapisha masharti haya ya mjadala. Halafu marafiki zangu wakawasili Qadian. Na kwa kuwa bwana Daktari ameupa mjadala huu jina la 'Vita Vitakatifu', hivyo mnamo tarehe 25 Aprili 1893 aliandikiwa kwamba masharti hayo ambayo marafiki zangu waliyakubali, mimi pia nimeyakubali. Lakini ni muhimu kwanza kupendekeza jambo hili kuwa vita hivi vitakatifu vitakuwa na athari ipi kwa pande mbili. Na itafahamika vipi kwa uwazi kabisa kuwa upande fulani kwa hakika umeshindwa, kwani kutokana na uzoefu wa miaka mingi jambo hili limeshathibitika kwamba ndani ya mijadala ya kiakili na kimaandiko hata kama upande fulani ushinde kwa uwazi kabisa, lakini watu wa upande wa pili kamwe huwa hawakubali kwamba wao kwa hakika wameshindwa. Bali wakati wa kuichapisha mijadala huongeza vielelezo vingi kwenye maandishi yao, wakijaribu kwamba kwa vyovyote ithibitike kuwa ushindi ni wao. Na kama mjadala ufanyike kwa hoja za kimaandiko tu, basi mwenye akili

anaweza akatabiri kuwa mjadala huu pia utakuwa kama ile mijadala iliyokuwa ikifanyika kati ya mapadri na wanazuoni wa Kiislamu. Bali kama itazamwe kwa undani basi ndani ya mjadala huo huwa hamuonekani jambo lolote lililo jipya. Kutoka kwa mapadri kutakuwa na ukosoaji ule ule wa kawaida, kwa mfano Islam imeenea kwa nguvu ya upanga, ndani ya Islam kuna mafundisho ya kuoa wake wengi, pepo ya Kiislamu ni pepo ya kimwili na kadhalika. Na hali kadhalika kutoka upande wetu pia yatatolewa, yale yale majibu ya kawaida kwamba Islam siyo iliyotangulia kunyanyua upanga na Islam ilinyanyua upanga wakati tu wa dharura kwa kustawisha amani tu. Na Islam haikutoa maagizo ya kuwaua wanawake, watoto na watawa wa dini. Bali wale waliotangulia kuinyanyulia Islam upanga hao tu wakauawa kwa panga. Na katika vita vya upanga mafundisho ya Taurati ndiyo yamezidi kuliko yote ambayo kwa sababu yake hata wanawake na watoto wasiohesabika waliuliwa. Yule Mungu ambaye machoni mwake vita zile zisizo na huruma na za kikatili hazikuwa mbaya, bali zilitokea kwa amri yake, basi itakuwa kinyume na uadilifu kuwa Mungu huyo huyo azikasirikie vita zile za Kiislamu ambazo Mtume mtakatifu wa Islam[saw] alilazimika kuzipigana katika hali ya kudhulumiwa au kwa lengo la kustawisha amani. Vivyo hivyo kuhusu shutuma za kuoa wake wengi, kutoka kwetu litakuwa lile lile jibu la kawaida kwamba kabla ya

Islamu kaumu nyingi zilifikia hata hatua ya kuoa wake wengi kwa mamia hata maelfu na Islam imepunguza idadi ya wake sio kuzidisha. Bali fadhila hii imo makhsus ndani ya Kurani tu kwamba imezikataa ndoa zisizo na mipaka na kikomo. Na wale manabii watakatifu wa kaumu ya Israeli ambao walioa wake mia moja, bali baadhi yao walifikia hadi wake mia saba, je walikuwa wakifanya uzinzi hadi mwisho wa uhai wao? Na je vizazi vyao, ambao baadhi yao walikuwa watu wema, bali hata walikuwa pia manabii, wanafahamika kuwa ni vizazi vya njia isiyo halali? Halikadhalika kuhusiana na pepo pia litakuwa ni lile lile jibu la kawaida kwamba pepo ya Waislamu sio pepo ya kimwili pekee, bali ni nyumba ambamo Mungu Ataonekana, na ni mahali pa aina zote mbili za wema wa kiroho na wa kimwili. Naam, Jahanam ya Wakristo ni ya kimwili tu.

Lakini hapa swali ni hili kwamba matokeo ya mijadala hii yatakuwa ni nini? Je twaweza kutumaini kwamba Wakristo watayakubali majibu haya ya Waislamu ambayo ni ya ukweli moja kwa moja na yenye msingi kwenye uadilifu? Au kwa ajili ya kumfanya mwanadamu kuwa Mungu miujiza pekee itatosha? Au zile ibara za Biblia ambamo minghairi ya kumtaja Hadhrat Masihi sehemu nyingine imeandikwa kwamba nyie nyote ni watoto wa Mungu, na sehemu nyingine imeandikwa kwamba nyie nyote ni mabinti Zake, na sehemu nyingine imeandikwa

kuwa nyie nyote ni miungu, itachukuliwa kwa maana ya dhahiri? Na kama hakuwezekani kuwa hivyo, basi mimi siwezi kufahamu kwamba matokeo bora ya mjadala huu ambao kwa ajili yake yalazimu kukaa Amritsar kwa siku 12, yatakuwa vipi.

Kwa kufikiria sababu hizo bwana Daktari alipewa shauri hili kwa njia ya barua iliyotumwa kwa rejista kwamba inafaa kuwa baada ya siku sita, yaani wakati kila upande kati ya pande hizi mbili utakapomaliza siku zake sita, basi uwepo baina yao Mubahala pia, nao utosheleze tu kwa kiasi hiki kwamba pande zote mbili ziombe kwa Mwenyezi Mungu ishara ya kimbingu kwa ajili ya kuisaidia dini yao na muhula wa mwaka mmoja uwekwe kwa ajili ya kudhihiri kwa ishara hizo. Halafu upande ule ambao ishara yoyote ya kimbingu idhihirike kwa ajili ya kuusaidia, ambayo ishara hiyo iwe zaidi ya uwezo wa mwanadamu, ambayo upande wa pili usiweze kukabiliana nayo, basi italazimika kwa upande ulioshindwa ufuate dini ya ule upande ambao Mwenyezi Mungu Ameushindisha kwa ishara Yake ya Kimbingu. Na kama utakataa kujiunga na dini, basi utawajibika kutoa nusu ya raslimali yake kwa upande ule ulioshinda, kwa kusudio la kuisaidia dini hiyo ya kweli. Hii ndiyo njia ambayo kwayo mpambanuo kamili utakuwepo baina ya haki na batili. Kwa sababu wakati wa kukabiliana na ishara ya kimuujiza, upande mwingine ukashindwa kabisa

kuonyesha ishara, basi ushindi wa upande ulioonyesha ishara utadhihirika kwa uwazi kabisa na hoja zote zitamalizika na ukweli utadhihirika. Lakini zaidi ya wiki moja imeshapita na hadi leo, yaani tarehe 3 Mei 1893, bwana Daktari hajaleta jibu lolote la barua hii. Kwa hiyo, kwa kupitia tangazo hili, bwana Daktari na kundi lake lote wanaombwa kwamba kwa kuwa waliuita mjadala huu kuwa 'vita vitakatifu' na wanataka uwepo uamuzi usio na utata kati ya Waislamu na Wakristo, na jambo hili lidhihirike kwamba Mungu wa kweli na Mweza ni Mungu wa nani, hapo kuwa na matumaini haya kwenye mijadala ya kawaida ni tamaa ya bure tu. Ikiwa dhamira hii ni yenye nia njema, basi hakuna njia yoyote iliyo bora ya hii kwamba sasa ukweli na uwongo ujaribiwe kwa msaada wa kimbingu, na mimi nimeikubali kwa dhati njia hii. Na njia ile ya mjadala wa hoja za kimaandiko na za kiakili iliyokubalika ingawa kwa rai yangu sio lazima sana, lakini hata hivyo nayo pia nimeikubali. Lakini pamoja na hayo, hili litakuwa ni miongoni mwa mambo ya lazima kwamba kila baada ya kumalizika miadi ya siku sita utafanyika Mubahala kati yangu na upande wa pili kwa njia iliyoelezwa hapo juu. Na pande zote mbili mapema ziyachapishe makubaliano haya kwamba tutafanya Mubahala. Yaani tutaomba dua kwa njia hii kwamba Ee Mungu Wetu, kama sisi tupo kwenye udanganyifu, basi dhihirisha kudhalilika kwetu kwa njia ya ishara ya

wapinzani wetu. Na kama sisi tuko kwenye ukweli, basi dhihirisha ishara ya kimbingu ya kutusaidia na kudhihirisha kudhalilika kwa wapinzani wetu. Na wakati wa dua hii pande zote mbili zitasema Amin. Na miadi yake itakuwa hadi mwaka mmoja. Na adhabu ya upande utakaoshindwa itakuwa hiyo iliyokwisha tajwa hapo juu.

Na kama litokee swali hili kwamba kama katika kipindi cha mwaka mmoja kusitokee ishara yoyote kwa kila upande au zitokee ishara kwa pande zote mbili, basi uamuzi utatolewaje? Basi jibu lake ni hili kwamba hata katika hali kama hii, mimi nitajifahamu kuwa nimeshindwa na nitakuwa ni mwenye kustahili adhabu ambayo imeshaelezwa. Kwa vile mimi nimetumwa toka kwa Mwenyezi Mungu na nimeshapata bishara ya ushindi, basi kama Mkristo yeyote akionyesha ishara ya kimbingu mbele yangu au mimi kwa mwaka mzima nisiweze kuionyesha, hapo kuwa kwangu kwenye batili kutadhihirika. Na ninaapa kwa Mungu Mwenye shani kwamba Mungu Mwenye shani Ameniambia kwa uwazi kabisa kwa njia ya Ufunuo kwamba Hadhrat Masihi[as] bila tofauti alikuwa ni mwanadamu tu kama walivyo wanadamu wengine, lakini yu Nabii wa kweli wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na mja Wake, na pia Akaniambia kwamba: "Kile alichopewa Masihi[as] umepewa wewe kwa kumfuata Nabii[saw]. nawe ndiye Masihi Mau'udi. Na pamoja nawe iko silaha yenye nuru

itakayoivunjilia mbali giza na itakayosadikisha bishara ya 'uvunjaji wa msalaba'."

Basi, kama jambo liko hivi, yalazimu kwa ajili ya ukweli wangu kwamba baada ya Mubahala lazima nidhihirikiwe na Ishara ndani ya mwaka mmoja. Na kama ishara isidhihirike, basi hapo mimi sikutoka kwa Mwenyezi Mungu, na sio tu nipate adhabu ile ile, bali nistahili kupata adhabu ya kifo. Basi leo mimi nikikubali mambo yote hayo nayatangaza. Sasa baada ya kulichapisha tangazo hili, yapasa na kuwajibika kwamba bwana Daktari naye atangaze kiasi hiki kwamba ikiwa baada ya Mubahala ishara yoyote ya kumsaidia Mirza Ghulam Ahmad, idhihirike ndani ya mwaka mmoja, ambapo kinyume chake ndani ya mwaka huo huo mmoja sisi tushindwe kuonyesha ishara, basi bila ya kusita tutaikubali dini ya Kiislamu, waila nusu ya mali yetu yote tutaitoa kwa upande ulioshinda kwa lengo la kuisaidia dini ya Islam, na siku zijazo kamwe hatutasimama kuipinga Islam. Wakati huu bwana Daktari atafakari kwamba mimi nimejiwekea masharti magumu sana na yeye nimemuwekea masharti rahisi. Yaani kama yeye aonyeshe ishara ile mbele yangu nami pia nionyeshe, hata hivyo, kwa mujibu wa sharti hili, yeye ndiye atakayechukuliwa kuwa mkweli. Na kama mimi nisiweze kuonyesha ishara wala yeye asiweze kuonyesha mpaka mwaka moja, hata hivyo yeye ndiye atakaye-chukuliwa

kuwa mkweli. Na mimi katika hali hii tu nitakubaliwa kuwa mkweli endapo kwa upande wangu ndani ya mwaka mmoja idhihirike ishara ambapo mbele yake bwana Daktari ashindwe. Na ikiwa baada ya kuchapisha tangazo hili, bwana Daktari asichapishe dhidi yake tangazo lenye madhumuni ya aina hii, basi hapo kukimbia kwake kutafahamika kwa uwazi kabisa. Nasi hata hivyo tunaweza kuhudhuria kwenye mjadala wake wa hoja za kimaandiko na za kiakili, sharti achapishe kuhusiana na habari hiyo, yaani yeye na watu wake kuwa wameshindwa mbele ya Islam katika suala la kuonyesha ishara, yaani aandike hivi kwamba hii ni shani ya Islam tu kwamba ishara ya kimbingu yadhihirika kwake na dini ya Kikristo haina baraka hizo. Nimepata kusikia kwamba bwana Daktari alisema haya pia mbele ya marafiki zangu kwamba: 'Sisi tutafanya mjadala huu, lakini mjadala huu utakuwa na dhehebu la Ahmadiyya, sio na Waislamu wa Jandyala.' Basi iwe wazi kwa bwana Daktari kwamba ni dhehebu la Ahmadiyya ndio walio Waislamu wa kweli ambao hawachanganyi rai za mwanadamu ndani ya maneno ya Mwenyezi Mungu, na wanakiamini cheo cha Hadhrat Masihi[as] kwa kiasi kile kile kinachothibitika ndani ya Kurani Tukufu.

*Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.*

## Tangazo kwa ajili ya kumpa taarifa bwana Batalawii

Iwe wazi kwamba bwana Sheikh Batalawii alifikishiwa mnamo tarehe 1 Aprili 1893 lile tangazo ambamo alialikwa kushindana kwa kuandika maelezo ya Kurani katika Kiarabu. Hivyo, bwana Mirza Khudaa Bakhsh, aliyekwenda Lahore kulipeleka tangazo hilo, alileta ujumbe huu kwamba bwana Batalawii ameahidi kuwa hadi wiki mbili kuanzia tarehe 1 Aprili atalichapisha jawabu na kulituma. Hivyo, nikalisubiri jibu kwa muda wa wiki mbili na hakuna jawabu lolote lililokuja. Halafu akakumbushwa tena, hapo akajibu hivi kwa njia ya barua ambayo imechapwa ndani ya kipeperushi changu kwamba: Sisi tutalichapisha jawabu na kulituma ndani ya mwezi huu huu wa Aprili. Sasa Aprili pia imepita na bwana Batalawii ametoa ahadi mbili na kuzivunja. Sisi hatumlaumu hata kidogo, lakini anapaswa aone aibu kwamba yeye bila ya uchunguzi wowote anawaita wengine waongo na wavunja ahadi, wakati yeye mwenyewe hazitekelezi kabisa ahadi zake. Inastaajabisha kwamba jawabu lile lingeweza tu kuwa ndio au hapana, lakini amepitisha mwezi mzima na mwezi huu umepotea bure tu tukisubiri. Sasa hata sisi tumefikiwa na kazi mbili muhimu: ya kwanza mjadala na Daktari Clark, pili, kuandika kijitabu kimoja cha muhimu ambacho

kitatumwa haraka huko Marekani kwa ajili ya kuusaidia Uislamu, ambayo maana yake itakuwa kwamba dini ya kweli na iliyo hai duniani ni Islam pekee. Hivyo, Bwana Batalawii anafahamishwa kwamba kama jibu lako litakuja kabla ya kazi hizo mbili kukamilika basi hatutakuwa na njia ila kutangaza tarehe nyingine kwa ajili ya kujadiliana nawe, itakayokuwa baada ya kumaliza kazi hizo mbili.

Leo nilipomaliza tu kuandika hilo tangazo, nikapata barua ya bwana Abdullah Atham iliyotumwa kwa njia ya posta. Barua hii ni jibu la barua ile niliyoiandika kuhusiana na mjadala uliotajwa hapa juu kwa bwana aliyetajwa na pia kwa bwana Daktari Clark. Sasa mimi naandika hapa chini jawabu lake kwa sura ya "Kauli yake" na 'Ninasema':

**Kauli yake**: Sisi hatukubali kwamba kuna haja ya mwujiza wowote mpya kwa ajili ya mafundisho ya kale. Hivyo hatuna haja ya mwujiza wala hatuoni uwezo ndani mwetu.

**Ninasema**: Rafiki yangu! Mimi sikutumia neno mwujiza ndani ya barua yangu. Bila shaka kuonyesha mwujiza ni kazi ya nabii na yule aliyetumwa kutoka kwa Mungu, sio ya kila mtu, lakini jambo hili mwaliamini na mwalifahamu kwamba kila mti hujulikana kwa matunda yake. Na matunda ya imani, kama vile yalivyotajwa ndani ya Kurani Tukufu ndivyo yalivyotajwa ndani ya Injili takatifu pia. Natumai kuwa utakuwa umeshafahamu, kwa hiyo hakuna haja ya kurefusha maneno. Lakini mimi nataka kujua kwamba je wewe huna uwezo hata wa kuonyesha tunda la kuwa na imani?

**Kauli yake**: Kwa hali zote, ikiwa mheshimiwa u tayari

kuonyesha mwujiza wowote ule, basi sisi hatutayafumba macho yetu kuutazama. Na masahihisho yoyote ya kosa letu tuwezayo kuyafanya kutokana na mwujiza wako basi sisi tutaifahamu hiyo kuwa faradhi yetu hasa.

**Ninasema**: Bila shaka kauli yako hii ina msingi kwenye uadilifu, na haiwezi kutoka kikamilifu toka kwenye kinywa cha yeyote yule asiye na wazo la uadilifu. Lakini sehemu hii, sentensi yako hii kwamba masahihisho yoyote ya kosa letu tuwezayo kuyafanya kutokana na mwujiza wako basi sisi tutaifahamu hiyo kuwa faradhi yetu hasa, yahitaji ufafanuzi. Mimi nimetumwa kwa kusudio hili tu kwamba ili niwafikishie ujumbe huu viumbe wa Mungu kwamba miongoni mwa dini zote zilzopo duniani, ile dini iliyoko kwenye ukweli na inayoafikiana na radhi ya Mwenyezi Mungu, ni ile iliyoletwa na Kurani Tukufu, na kwa ajili ya kuingilia ndani ya nyumba ya wokovu, mlango wake ni:

لَا إِلٰهَ إِلَّا اللهُ مُحَمَّدٌ رَسُوْلُ اللهِ [7]

basi tu. Sasa je upo tayari kuikubali dini hii baada ya kuiona ishara? Sentensi yako iliyotajwa hapo juu yanipa matumaini kwamba hutaikataa. Hivyo, kama u tayari basi chapisha mistari michache ndani ya magazeti matatu,

---

[7] Hapana apasaye kuabudiwa ila Allah na Muhammad ni mtume wa Allah. (Mwenezi)

yaani la *Nuur Afshaan*, *Manshuur Muhammadi* na ndani ya gazeti lolote la Mwaria kwamba sisi kwa kumjua Mungu kwamba Yupo na kwamba Anaona, twatoa ahadi hii, kwamba ikiwa baada ya mjadala huu ambao umekubaliwa kufanyika tarehe 22 Mei 1893, Mwenyezi Mungu Amsaidie Mirza Ghulam Ahmad na Mwenyezi Mungu Adhihirishe ishara yoyote ile kwa kumsaidia, ambayo yeye awe ameitaja kabla ya wakati wa kutokea nayo pia itimie sawa sawa na usemi wake, basi baada ya kuiona ishara hiyo tutasilimu bila ya kusita. Nasi twaahadi hii pia kwamba tutaikubali ishara hiyo bila ya aina yoyote ile ya ukosoaji wa hovyo, na katika hali yoyote ishara hiyo haitafahamika kuwa hafifu na yenye kustahili kukosolewa, pasipokuwa na sharti kwamba sisi pia tuonyeshe ishara ya aina hii hii ndani ya mwaka mmoja. Kwa mfano, kama kwa namna ya Ishara uwepo utabiri huu kwamba wakati fulani, mtu fulani makhsus au kundi fulani litapatwa na janga fulani, na utabiri huo utimie katika muda huo, basi bila ya kutoa mfano wa utabiri huo kwa upande wetu kwa hali yoyote ile italazimika kukubaliwa utabiri huo. Na kama sisi, baada ya kuiona ishara, tusijiunge na dini ya Islam wala kuikabili tusiweze kuonyesha ishara kinyume cha kwaida kama hiyo hiyo ndani ya mwaka mmoja, basi kwa adhabu ya kuvunja ahadi tutaikabidhi kwake nusu ya mali yetu kwa ajili ya kuisaidia Islam. Na kama sisi tusiutekeleze sehemu hii ya

pili pia na kuivunja ahadi, hapo kama baada ya uvunjaji huu wa ahadi, Mirza Ghulam Ahmad atake kuchapisha ishara yoyote ya adhabu kali dhidi yetu, basi atakuwa na ruhusa kutoka kwetu kuichapisha kwa jumla kwa njia ya magazeti au katika majarida yake yanayochapishwa. Basi maandishi yako tu haya yaambatane na jina, dini, ubini na maskani, na ushahidi wa mashuhuda hamsini wenye kuheshimika na kuaminika toka kila upande uwepo juu yake, ndipo uzichapishe ndani ya magazeti matatu. Kwa kuwa matashi yako ni kudhihirisha ukweli, na kipimo hiki chaafikiana na dini yenu na yetu, hivyo sasa, kwa ajili ya Mungu, usisite kukikubali. Sasa kwa hali yoyote ile wakati ule umefika kwamba Mungu Adhihirishe nuru na baraka za dini ya kweli na Aifanye dunia iwe katika dini moja tu. Basi, kama uuimarishe moyo wako na kuwa wa kwanza kabisa kupiga hatua ndani ya njia hii na halafu uitimize pia ahadi yako kwa ukweli na ushujaa, basi mbele ya Mwenyezi Mungu utahesabika kuwa ni mkweli, na hii daima itakuwa ni alama ya ukweli wako.

Na kama useme kwamba "Sisi tutayatekeleza mambo yote haya na baada ya kuiona ishara yoyote ile tutaikubali Islam au tutayatekeleza masharti mengine yaliyotajwa hapo juu, na ahadi hii mapema tutaichapisha pia ndani ya magazeti matatu, lakini kama wewe ndiye utakayetokea kuwa mwongo na kutoweza kuonyesha ishara yoyote basi utapewa adhabu gani," basi jibu langu ni kuwa mimi sawa

na matashi ya Taurati, nitakubali kupata adhabu ya kifo; na hii ikiwa kinyume na sheria ya nchi, basi mimi nitakupa mali yangu yote. Kwa vyovyote utakavyo uchukue dhamana yangu mapema.

**Kauli Yake**: Lakini, Bwana, ukumbuke kwamba sisi tutautambua ule tu kuwa mwujiza utakaodhihirika baada ya *tahaddi* ya mdai mwujiza yaani kwa kusisitiza kwamba lazima utatokea na utakaokuwa unasadikisha jambo fulani linalowezekana.

**Ninasema**: Nilikubali hilo. Na *tahaddi* humaanisha kwamba, kwa mfano, mtu fulani akidai kuwa anatoka kwa Mungu atoe bishara yoyote ile kwa ajili ya kusadikisha madai yake, iliyo nje ya uwezo wa mwanadamu, na bishara hiyo itimie, hapo huyo atahesabiwa kuwa ni mkweli sawa na maagizo ya Taurati, Kumbukumbu la Taurati 18:18. Naam, hii ni kweli kwamba ishara ya aina hiyo ni lazima iwe yenye kusadikisha jambo fulani linalowezekana. Waila hii haijuzu kwamba mtu fulani, kwa mfano, aseme kwamba 'mimi ni Mungu' na katika kuthibitisha uungu wake atoe bishara yoyote na bishara hiyo itimie basi halafu aaminiwe kuwa ni Mungu.

Lakini mimi sehemu hii nataka nikuulize kwamba wakati nilipotoa madai ya kupokea ufunuo na kutumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi mnamo mwaka 1888, Mirza

Imamud Diin, ambaye wewe wamtambua vema, alichapisha tangazo dhidi yangu ndani ya *Chashmae Nuur* la huko Amritsar na kuniomba nionyeshe ishara. Hapo kwa ajili ya kudhihirisha ishara, bishara fulani ilitolewa iliyochapishwa ndani ya *Nuur Afshaan* la tarehe 10 Mei 1888, ambayo maelezo yake kwa kirefu yamo ndani ya gazeti hili na pia yamo ndani ya ukurasa wa 279-280 wa kitabu changu cha *Aina Kamaalaate Islam*. Na bishara hiyo ilitimia ndani ya muda wake mnamo tarehe 30 Septemba 1892. Hivyo sasa, kwa njia ya kuupima uadilifu wako, ninakuuliza kwamba je hii ni ishara au siyo? Na kama sio ishara, basi sababu yake ni nini? Na kama ni ishara, na wewe umeiona pia, na sio tu imeshachapishwa katika *Nuur Afshaan* la tarehe 10 Mei 1888, bali hata ndani ya tangazo langu lililotolewa mnamo tarehe 10 Julai 1888 imekwisha chapishwa pamoja na muda wake. Hivyo hebu sema kwamba je, sasa ni faradhi yako au la kwamba ufaidike na ishara hii pia na urekebishe kosa lako. Na tafadhali unifahamishe kuwa umejirekebisha vipi, na kwa namna gani umeachana na msingi wa Kikristo. Kwa sababu ishara hii sio ya zamani sana, ni tukio la karibuni tu lililochapishwa ndani ya *Nur Afshaan* na ndani ya tangazo langu la tarehe 10 Julai 1888, na hii inaafikiana na masharti yako yote. Kwa rai yangu, hiki ni kipimo kimoja cha uadilifu wako. Ikiwa umeikubali ishara hii, na sawa na kukiri kwako

umerekebisha pia kosa lako, basi mimi nitakuwa na yakini imara kwamba sasa kwa siku zijazo pia uko tayari kujirekebisha sana. Unapaswa kuwa na athari ya ishara hii kwa angalau kiasi hiki kwamba, kwa uchache, uchapishe kukiri kwako huku kwamba ingawa bado sijaamini hasa lakini dhana yangu kubwa ni kwamba dini ya Islam ndiyo ninayoiona kuwa ya kweli, kwa sababu bishara iliyotolewa kama changamoto kwa ajili ya kumsaidia ilitimia. Wewe wafahamu kuwa Imamud Diin anaikana Islam na hamwamini Mungu, na kwa njia ya tangazo aliomba ishara ya ukweli wa Islam na ya kupokea kwangu Wahyi, ambayo Mwenyezi Mungu Akiwatilia hiyo jamaa zake kwa njia ya karibu na kutimiza hoja kwake. Ni lazima utoe jibu la kuikataa au kuikubali ishara hii waila hili litakuwa ni deni letu la kwanza kwako.

**Kauli Yake**: Hata Mibahala ni aina ya miujiza, lakini sisi, sawa na mafundisho ya Injili hatuwezi kumwombea mtu yeyote laana. Wewe unayo hiari ya kuomba chochote utakacho na kulisubiri jibu hadi mwaka mmoja.

**Ninasema**: Rafiki yangu! Ndani ya Mubahala hamna ulazima wa kuwalaani wengine, bali yatosha tu kusema hivi kwamba, kwa mfano Mkristo aseme kuwa mimi ninasema kwa yakini kamili kwamba kwa hakika Hadhrat Masih ni Mungu na Kurani haikutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kama mimi ni mwongo katika usemi wangu

huu basi Mwenyezi Mungu Anilaani. Hivyo sura hii ya Mubahala haipingani na Injili bali yaafikiana kabisa, isome Injili kwa makini.

Mbali na hayo, mimi nimeshaandika hapo awali kwamba kama wewe washindwa kufanya mashindano ya kuonyesha ishara, basi yawepo ya upande mmoja tu wa kwangu, mimi nakubali kwa moyo mkunjufu kabisa. Wewe chapisha kukubali kwako sawa na mfano wa ilivyoandikwa hapo juu, na wakati wowote utakaosema, mimi bila kusita nitahudhuria Amritsar. Mimi tokea mwanzo tu ninafahamu kuwa dini ya Kikristo iliingia gizani siku ile ile Hadhrat Masih[as] alipopewa nafasi ya Mwenyezi Mungu, na Wakristo walipomkataa nabii mkweli, mkamilifu na mtakatifu, aliye mbora wa manabii, Muhammad Mteule[saw]. Hivyo mimi ninafahamu kwa yakini kuwa miongoni mwa Wakristo hamna yeyote mwenye uwezo wa kushindana na nuru zenye uhai za Islam. Mimi naona kwamba ule wokovu na uhai wa milele unaotamkwa na Wakristo, huo unang'aa kama jua ndani ya watu waliokamilika kati ya Waislamu. Hii ni sifa kubwa sana makhsus ndani ya Islam kwamba baada ya kutoa kutoka katika giza yaingiza ndani ya nuru yake — nuru ambayo kutokana na baraka yake athari za wazi wazi za kukubalika huzalika ndani ya mwaminio, na heshima ya kuongea na Mwenyezi Mungu hupatikana, na Mwenyezi Mungu Hudhihirisha ndani yake ishara za

mapenzi Yake. Hivyo kwa nguvu nasema na kudai kuwa uhai wa kiimani anaupata Mwislamu tu aliyekamilika, na hii ndiyo alama ya ukweli wa Islam.

Sasa jibu la muhimu la barua yako limeshatolewa. Na tangazo hili katika sura ya kijitabu nakutumia wewe na pia Dr. Clark kwa njia ya rejesta. Basi, hoja imeshatimia kwa upande wangu, na sasa unayo hiari.

*Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.*
Mwandishi, Mnyenyekevu,
Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian,
Wilaya ya Gurdaspur.

## Bishara moja kumhusu sheikh Muhammad Husein Batalawii

Siku hizi, Sheikh Muhammad Husein Abu Said yuko katika hali ya hatari sana. Mtu huyu ananifahamu mimi kuwa ni kafiri, na sio kafiri tu bali ndani ya fatuwa yake ya kufuru masheikh wengi wametumia neno la Akfar pia (kafiri mkubwa kabisa) kuhusiana nami. Amemwingiza hata mwalimu wake kikongwe, Nazir Husein wa Delhi, ndani ya balaa hili hili. Subhanallah! Mtu ambaye anamwamini Mungu Mwenye Shani na anamwamini Mtume Wake Mtukufu[saw]. na anashikamana na saumu na sala, naye yu miongoni mwa wanaokielekea Kibla na katika matendo yake yote hapingani hata kidogo na Kitabu cha Mungu na Suna za Mtume[saw]. wa Mungu, Sheikh Batalawii anasema mtu huyo kuwa ni kafiri bali kafiri mkubwa kabisa atakayedumu ndani ya Jahanam milele kwa sababu hii tu kwamba yeye anamfahamu Hadhrat Masih[as] kuwa mfu kwa mujibu wa maneno ya waziwazi ya Kurani فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي[8], na kwamba kwa mujibu wa bishara ya Mtume[saw]. Masihi Mau'udi atatokana na umati huu huu, na kwa msingi wa funuo zinazomteremkia mara kwa mara na ishara za wazi kabisa anajidhihirisha kuwa ni Masihi Mau'udi. Na Sheikh Batalawii, kwa njia ya uzushi

[8] Al-Maaida, 5:118. (Mwenezi)

anasema hivi pia kuwa kana kwamba mimi nawakana Malaika na kuikataa Miraji ya Mtume[saw]. na ninadai unabii na pia siamini miujiza. Subhanallah! Huyu masikini amezua uzushi kiasi gani kwa ajili ya kukufurisha. Anafia ndani ya huzuni hizo hizo kwamba kwa hali yoyote ile viumbe wa Allah wamuelewe Mwislamu mmoja kuwa ni kafiri, bali wamseme kuwa amewazidi hata Wakristo na Mayahudi katika kufuru. Waliomwona wanasema kuwa sasa hali ya mtu huyo ni mbaya sana. Kama mtu kwa bahati akipata kusema, "Bwana! kwa nini wamkufurisha mtu anayetoa shahada? Hebu mwogope Mungu", basi humchagiza mtu huyo kama mwenye kichaa na akinitukana sana anasema, "Lazima yu kafiri na mbaya zaidi kuliko makafiri wote". Nawaomba wale wanaomtakia heri kwamba ni lazima wamwombee dua katika wakati huu wa hatari. Hivi sasa merikebu yake imo ndani ya kizingia cha maji ambamo kuokoka inaonekana kuwa ni muhali. *Na kwa hakika niliota kwamba mtu huyu ataiamini imani yangu kabla ya mauti yake na niliota kana kwamba ameiacha kauli ya kukufurisha na ametubu. Na hii ndiyo ruya yangu, na ninataraji Mola wangu Ataifanya kuwa ya kweli. Na amani iwe juu ya yule aliyefuata mwongozo.*

Mwandishi, mnyenyekevu,
Ghulam Ahmad kutoka Qadian, wilaya ya Gurdaspur,
4 Mei 1893

اَلْحَمْدُ لِلّٰہِ نحمدہٗ و نستعینہٗ و نصلی علیٰ رسولہ الکریم [9]

Kwa Bwana Mheshimiwa, Mwenye baraka, Mujaddidi wa zama, Mwanazuoni aliyebobea, mwenye kuihami dini ya Mtume[saw]., Hadhrat Ghulam Ahmad sahib, toka kwa Muhammad Bakhsh

*Assalaamu Alaikum*!

Ningependa kueleza kwamba tangu muda kadha Wakristo wa mji mdogo wa Jandyala wanaendelea kupiga kelele nyingi na kuzua tafrani, bali leo hii, tarehe 11 Aprili 1893, Wakristo wa Jandyala, kwa kupitia kwa Dr. Martyn Clark wa Amritsar wamenitumia barua ya rejista ambayo nainakili upande wa pili wa barua hii uipitie. Wakristo wameandika kwa kusisitiza na kukazania sana kwamba Waislamu wa Jandyala wafanye mkutano wa hadhara kwa kuwahudhurisha wanachuoni wao na wazee wengine wa dini na ufanyike utafiti wa dini ya kweli, waila katika siku zijazo itabidi wanyamaze kuuliza maswali. Kwa hiyo nakuomba wewe mwenye baraka kwamba kwa kuwa Waislamu wa Jandyala wengi wao ni dhaifu na maskini, hivyo nakuomba wewe mtukufu kwamba tafadhali uwasaidie Waislamu wa Jandyala kwa ajili ya Allah tu; la sivyo, Waislamu watapata doa. Na pia baada ya kuipitia

[9] Sifa zote njema zinamhusu Allah na tunamhimidi Yeye, na Yeye twamuomba msaada, na twamsalia mtume Wake mkarimu. (Mwenezi)

barua ya Wakristo uandike kwamba waandikiwe nini katika kuwajibu barua yao. Jinsi utakavyoagiza ndivyo hivyo hivyo itakavyotekelezwa. Basi.

Tafadhali utujibu lazima.

Mwandishi,
Muhammad Bakhsh Pandah wa Maktab Desi, mji wa Jandyala, wilaya ya Amritsar, 11 Aprili 1893

## Kwa mheshimiwa bwana Mian Muhamad Bakhsh na kwa Waislamu wote wa Jandyala[10]

Mheshimiwa wangu, baada ya salamu rai yako tukufu iwe wazi kwamba, kwa kuwa siku hizi katika mji wa Jandyala kuna maongezi mengi ya kidini kati ya Wakristo na Waislamu na baadhi ya watu wachache wa dini yako wanaikosoa dini ya Kikristo na kuna wengine wengi wanaojadiliana na kutaka kuendelea. Na kadhalika Wakristo nao wamefanya tafiti nyingi kuhusu dini ya Muhammad na mambo yapo karibu kupita kiasi. Hivyo kwa rai ya mwandishi wa barua hii njia bora na yenye kufaa inayoonekana ni hii kwamba ufanywe mhadhara ambamo wawepo Waislamu wanazuoni pamoja na wazee wengine wenye kutegemewa na hali kadhalika kwa upande wa Wakristo waletwe wenye kutegemewa ili zile hitilafu zilizopo siku hizi ziamuliwe vizuri, na ubainike wema na uovu, na ukweli na ulio kinyume chake. Hivyo, kwa kuwa baina ya Waislamu wa Jandyala wewe unafikiriwa kuwa mwenye hima, sisi kwa niaba ya Wakristo wa Jandyala twakuomba kwamba wewe mwenyewe, au baada ya kushauriana na watu wa dini yako, uchague wakati fulani na umwite mkubwa yeyote

---

[10] Ile barua ambayo Dr. Martyn Clark alimuandikia Bwana Muhammad Bakhsh Pandah. (Mwenezi)

unayeridhika naye, nasi pia katika wakati huo uliopangwa tutamleta yeyote kati yetu katika hafla hiyo tukufu, ili mhadhara ufanyike na uamuzi wa mambo yaliyotajwa hapo juu pia ufanyike vyema, na Mungu Awapatie wote njia iliyonyooka. Sisi hatuufuatilii mhadhara huu kwa mtazamo wowote ule wa kukazana au ufisadi au upinzani, bali kwa msingi huu tu kwamba yale mambo ya uongofu, ya ukweli na yenye kupendeza yadhihirike vema kwa watu wote. Ombi lingine ni hili kwamba ikiwa Waislamu hawapendi kushiriki kwenye mjadala huu, basi siku zijazo wasiingilie kati uwanja wa mazungumzo na wakati wa mahubiri au katika fursa zingine wajiepushe kutoa hoja zisizo na msingi na zisizofaa na wanyamanze. Tafadhali toeni haraka jibu la barua hii ili kama mkikubali ombi letu hili, uandaliwe utaratibu unaofaa wa huo mkutano na yale madhumuni ambayo kwayo mjadala utafanyika. Basi. Salamu nyingi. Nakala hii ni kama barua yenyewe.

Mwaandishi, Wakristo wa Jandyala, Martyn Clark wa Amritsar. Saini katika Kiingereza.

## Nakala ya Barua toka kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad kwa Wakristo wa Jandyala. Ilitumwa kwa rejista mnamo tarehe 13 Mei 1893

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [11]

Kwa Wakristo wa Jandyala

Baada ya kuamkia, leo nimeyasoma mliyomwandikia bwana Mian Muhammad Bakhsh kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ninaafikiana na yale mliyofikiria, bali kwa hakika nilifurahi sana kwa kuyasoma madhumuni hayo hata kwamba siwezi kuieleza hali hiyo ndani ya barua hii fupi. Ni kweli, na ni kweli kabisa, kwamba magomvi haya ya kila siku sio mazuri, na kutokana nayo siku hadi siku uadui unazidi na amani na utulivu kati ya pande mbili huharibika. Lakini jambo hili ni la kawaida tu, bali lililo muhimu sana kuliko hilo na kustahili kutajwa ni kwamba kwa kuwa watu wa pande zote mbili hawana budi kufa na kuiacha dunia, basi kama hawadhihirishi ukweli kwa kufanya mjadala, watakuwa wanajidhulumu nafsi zao na wengine. Sasa mimi naona kwamba Waislamu wa Jandyala hawana haki zaidi kuliko mimi bali kwa kuwa Mungu Mkarimu na Mwenye Huruma Amenituma kwa kazi hizo hizo, basi itakuwa ni dhambi kubwa kwamba

[11] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. (Mwenezi)

nikae kimya katika fursa kama hii. Kwa hiyo ninawaarifuni kwamba mimi tu nipo kwa kazi hii. Hii ni dhahiri kwamba pande zote mbili zina madai haya kwamba wamepata dini zao toka kwa Mwenyezi Mungu kwa ishara nyingi sana. Na pia pande mbili zinakubali kwamba dini inayoweza kuwa hai ni ile tu ambayo dalili zilizo msingi wa ukweli wake, dalili hizo zisiwe hadithi tu bali ziwepo hata sasa zikiwa dalili na ziwe wazi. Kwa mfano, ikiwa ndani ya kitabu fulani imeelezwa kwamba nabii fulani aliwaponya wagonjwa wa aina kadha wa kadha kimwujiza, basi jambo hili na mambo mengineyo ya aina hii hayawezi kuwa dalili ya wazi na ya yakini kwa ajili ya watu wa zama hizi, bali ni habari tu ambayo kwa mtazamo wa wenye kukataa yaweza kuwa ya ukweli na ya uwongo. Bali mwenye kukataa ataifahamu habari kama hizo kuwa ni kisa tu. Na hii ndiyo sababu kwamba wanafalsafa wa Ulaya hawawezi kufaidika hata kidogo na miujiza ya Masihi iliyoandikwa ndani ya Injili, bali huangua kicheko kuisikia. Kama ni hivyo, basi huu ni mjadala rahisi sana, nao ni hivi kwamba Mwislamu mmojawapo ajithibitishe nafsi yake kuwa yu sawa na mafunzo na zile alama zilizomo ndani ya Kurani kwa ajili ya Mwislamu aliyekamilika; na asipoweza, basi yu mwongo, sio Mwislamu. Kadhalika miongoni mwa Wakristo mtu mmojawapo ajithibitishe kuwa yu sawa na alama zile zilizomo ndani ya Injili; na kama asiweze

kuthibitisha basi huyo ndiye mwongo, sio Mkristo. Kwa kuwa pande zote mbili zinadai kuwa nuru ile waliyoleta manabii wao haikuwa yenye kuishia hapo tu bali ilikuwa yenye kuendelea, hivyo katika dini ile ambamo nuru hiyo itathibitika kuwa ni yenye kuendelea, basi kuhusiana na dini hiyo tu akili itatoa rai kuwa dini hiyo ndiyo iliyo hai na ya kweli. Kwa sababu, ikiwa sisi kwa njia ya dini fulani hatuwezi kuupata uzima ule na nuru ile takatifu inayonasibishwa kwake pamoja na alama zake zote, basi dini hiyo inakuwa si chochote zaidi ya majitapo tu. Kama tuseme kwamba Nabii fulani alikuwa mtakatifu lakini hawezi hata kumtakasa yeyote kati yetu, na alikuwa ni mwenye miujiza lakini hawezi kumfanya yeyote kuwa mwenye miujiza, na alikuwa ni mwenye kupokea ufunuo lakini hawezi kumfanya yeyote kati yetu kuwa mwenye kupokea ufunuo, basi nabii kama huyu anatufaa nini? Lakini sifa zote njema na hisani zote ni za Mungu kwamba bwana wetu na Mtume wetu aliye Muhuri wa Manabii, Muhammad Mteule[saw]. hakuwa hivyo. Yeye aliwapa watu wengi sana sawa na viwango vya madaraja yao ile nuru aliyopata, naye alitambuliwa kutokana na ishara zake zenye nuru. Yeye alikuwa nuru kwa kudumu milele aliyetumwa. Na kabla yake hakuja yeyote yule kuwa nuru wa milele. Kama yeye asingekuja na asingefahamisha basi sisi tulikuwa hatuna dalili yoyote ya unabii wa Hadhrat Masihi[as], kwa sababu dini yake ilikuwa

imekufa na nuru yake ilikuwa haina alama na hakukuwepo mrithi wake yeyote aliyepewa sehemu ya nuru hiyo. Sasa dini iliyo hai duniani ndiyo Islam tu. Nami nimeona na kuchunguza kwa uzoefu wangu binafsi kwamba aina zote mbili za nuru hadi sasa zipo kwa upya wake ndani ya Kurani na ndani ya Islam kama zilivyokuwepo wakati wa zama za Nabii wetu[saw]. na ni jukumu letu kuzionyesha. Kama kuna yeyote mwenye nguvu ya kushindana, basi na aandikiane nasi. Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.

Mwishoni, hii pia iwe wazi kwamba yule mtu atakayesimama kujadiliana nami ni lazima awe miongoni mwa wazee mashuhuri na miongoni mwa mapadri wazungu wenye kuheshimika, kwa sababu jambo lililokusudiwa katika mashindano au mjadala huu na ambalo imekusudiwa athari yake kuingizwa kwa watu wa kawaida, linalitegemea jambo hili kwamba washindani wa pande mbili wawe miongoni mwa wakuu wenye kuwaathiri watu wa kawaida. Naam, kwa kulegeza na kwa kutimiza hoja, mimi pia nakubali kwamba kwa ajili ya mashindano haya, achaguliwe kutoka kwa Wakristo, Padri Imaduddiin au Padri Thakar Das au bwana Abdullah Atham, na halafu majina yao yachapishwe katika gazeti mojawapo na nakala yake moja itumwe kwangu pia, na baada ya kuletwa hiyo nakala mimi nami nitatoa tangazo la kushindana, na gazeti moja nitalituma

kwa mshindani. Lakini iwe wazi kwamba kwa muda mrefu kumekuwepo na mzozo wa aina hii kati ya Waislamu na Wakristo na tangu hapo mijadala ikawepo na vitabu vingi sana vikaandikwa na pande hizo mbili. Na kwa hakika wanazuoni wa Kiislamu walithibitisha kwa uwazi kabisa kwamba lawama zozote zinazotolewa juu ya Kurani, hizo kwa namna nyingine zinakuwa ni lawama juu ya Taurati. Na shutuma zozote zilizotolewa dhidi ya shani ya Nabii wetu[saw], hizo kwa namna nyingine zinakuwa ni shutuma dhidi ya shani ya manabii wote ambazo hata Hadhrat Masihi hayuko nje yake, bali kwa sababu ya shutuma za aina hii hata Mwenyezi Mungu Anakuwa ni mwenye kurejewa na shutuma. Kwa hiyo mjadala huu utakuwa kuhusu kuchunguza dini iliyo hai au ile iliyokufa. Na itatazamwa kwamba zile alama za kiroho zilizodaiwa na dini na kitabu hicho hata sasa zapatikana ndani yake au la? Na itafaa kwamba sehemu ya kufanyika mjadala huo iteuliwe kuwa ni Lahore au Amritsar, na mjadala huo ufanyike ndani ya mjumuiko wa wanazuoni wa pande mbili.

Mnyenyekevu,
Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian
Wilaya ya Gurdaspur

Mheshimiwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Ukae salama,

Ama baada ya salamu, barua yako imewasili. Baada ya kuisoma nikafurahi, hasa kutokana na jambo hili kwamba Waislamu wa Jandyala wamempata bingwa na stadi kama wewe. Lakini kwa kuwa hatukukutupia mwito wewe bali Waislamu wa Jandyala, basi sisi hatuwezi kuukubali mwito wako. Tumeshawaandikia barua na hadi sasa twasubiri jibu. Kama utakubali kuwasaidia basi njia ifaayo na ya kawaida ni hii kwamba wewe mwenyewe uwaandikie barua, uwadhihirishie makusudio yako ya kuwasaidia. Kama wao wakikukubali na kukuteua wewe kwa ajili ya vita hivi vitakatifu, basi sisi hatuna udhuru wowote bali tutafurahi kabisa. Kwa kuwa u mwema na mwenye uzoefu, haitakuwa imefichika kwako kwamba kwa ajili ya mjadala huu makhsus kukukubali wewe au kutokubali si hiari yetu bali ndiyo ya Waislamu wa Jandyala. Hivyo, fanya nao uamuzi, nasi tupo tu, kukawia ndiyo kwa kusubiri uamuzi wako na wao. Salamu nyingi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ[12]

Bwana Padri mpendwa, mkarimu,

Baada ya yanayowajibika, wenye baraka ulioje wakati huu kwamba mimi nikiwa tayari kwa vita hivi vitakatifu ulivyovitaja ndani ya barua yako nawatuma marafiki zangu wachache niliowachagua waende kwako kama wawakilishi wangu, nami natumai utanikubali mimi nipambane katika vita hivi vitakatifu. Nilipoipata barua yako ya kwanza uliyowaandikia baadhi ya Waislamu wa Jandyala na kuzisoma ibara hizi kwamba je kuna yeyote wa kupambana nasi, basi papo hapo roho yangu ikatamka, "Naam mimi nipo, ambaye kwa mkono wake Mwenyezi Mungu Atawapa ushindi Waislamu na kuudhihirisha ukweli." Ule ukweli nilioupata na lile jua lililochomoza miongoni mwetu sasa halitaki kujificha. Mimi naona kwamba sasa litatoka kwa miale yenye nguvu sana na litaiathiri mioyo na kuvutia upande wake. Lakini kwa ajili ya kuchomoza kwake kuliihitaji fursa, basi kuwaita kwenu Waislamu kwenye mapambano ndiyo fursa iliyobarikiwa na njema mno. Sitarajii kwamba utang'ang'ania kwamba eti sisi twahusika

[12] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. (Mwenezi)

tu na Waislamu wa Jandyala na sio na wengine. Wewe wafahamu kwamba katika Jandyala hakuna yeyote aliye mwanazuoni mashuhuri na mwenye jina, na hata hii itakuwa mbali na shani yako kwamba uzozane na watu wa kawaida. Na hali yangu haijafichika kwako kwamba ninayo kiu ya miaka kumi ya kushindana nanyi na nimeshatuma maelfu ya barua kwa Kiurdu na Kiingereza kwa Mapadri waheshimiwa kama wewe kutokana na jadhba ya kiu. Lakini lisipokuja jibu lolote nikakata matumaini na kujikalia. Kama mfano ninazituma hata baadhi ya barua hizo, ili upate kufahamu kuwa mstahiki wa kwanza wa mwelekeo wako huu ndimi mimi tu. Waila kama mimi ni mwongo basi niko tayari kupokea kila adhabu. Kwa miaka kumi kamili nimesimama uwanjani. Ninavyofahamu hakuna hata mmoja huko Jandyala anayeweza kudhaniwa kuwa ni askari wa kusimama uwanjani. Hivyo najikalifisha kwa adabu kuwa kama jambo hili lahitajika kwamba magomvi haya ya kila siku yaishie, na ile dini ambayo Mungu yu pamoja nayo, na wale watu wanaomwamini Mungu wa Kweli zidhihirike nuru zao za kupambanua, basi yafanyike mashindano na mimi. Dai lenu kubwa ni kwamba Hadhrat Masihi[as] alikuwa kwa hakika Mungu, naye ndiye alikuwa mwumba wa mbingu na ardhi; nasi

twasema kwamba yeye kweli alikuwa nabii, alikuwa mtume, alikuwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu, lakini hakuwa Mungu. Hivyo, mashindano haya yatakuwa kwa ajili ya uamuzi wa kweli wa mambo haya haya. Mwenyezi Mungu Amenipasha habari moja kwa moja kwamba yale mafundisho yaliyoletwa na Kurani ndiyo hayo hayo yaliyo njia ya ukweli. Tauhidi hiyo hiyo takatifu ndiyo ambayo kila nabii aliwafikishia umati wake, lakini pole pole watu wakakengeuka na binadamu wakapewa nafasi ya Mwenyezi Mungu. Ilmuradi, mjadala utakuwa juu ya suala hili hili. Nami nina yakini kwamba ule wakati umefika ambapo ghera ya Mwenyezi Mungu itaonyesha kazi yake. Nami natumai kwamba kutokana na mashindano haya matokeo yenye faida na athari yatatokea kwa ajili ya dunia, na si ajabu kwamba sasa dunia nzima au sehemu yake kubwa ikaikubali dini moja tu iliyo ya ukweli na iliyo hai, na wale ambao unaandamana nao wingu la ukarimu wa Mwenyezi Mungu. Yatakiwa kwamba mjadala huu usiishie tu ardhini, bali mbingu pia ishiriki humo. Na mashindano yawe kuhusu hili tu kwamba uhai wa kiroho, mkubaliko wa kimbingu na busara vimo ndani ya dini ipi. Na mimi na mshindani wangu tuthibitishe ndani ya nafsi zetu zile athari za vitabu vyetu. Naam, kama wapende kwamba

baadaye hata kwa hoja za kiakili pia itikadi zote hizi mbili zitatuliwe, basi hiyo pia ni bora, lakini kabla ya hiyo majaribio ya kiroho na ya kimbingu ni lazima yawepo.

*Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.*
Mnyenyekevu,
Ghulam Ahmad Qadian
Wilaya ya Gurdaspur, tarehe 23 Aprili, 1893

Amritsar (24 Aprili 1893) — Tafsiri ya barua ya Bw. Dr. Clark

Kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad Chifu wa Qadian

Mheshimiwa wangu, amefika hapa Maulawii Abdul Karim akiwa pamoja na wawakilishi wako waheshimiwa na kunipa barua yako uliyotuma kwa mkono wake. Mwito ulionitupia kwa niaba ya Waislamu kwa ajili ya mashindano ninaukubali kwa furaha. Sawa na rai yako tumeshafanya uamuzi wa mjadala na masharti yake muhimu, na nina yakini kwamba nawe pia utayakubali mpango huo na masharti. Hivyo, tafadhali, upatapo fursa unifahamishe kama umekubaliana na masharti hayo au la.

Wako mtiifu,
H. Martyn Clark, M.D.C.M. (Edinburg)M.R.A.S.C.M.S.

## Masharti ya mpango wa mjadala yaliyokubaliwa baina ya Wakristo na Waislamu[13]

1. Mjadala huu utafanyika Amritsar.

2. Ni watu hamsini tu watakaohudhuria toka kila upande. (i) Bwana Mirza Ghulam Ahmad atawapatia Wakristo tiketi hamsini, na Dr. Clark atatoa tiketi hamsini kwa Bwana Mirza kwa ajili ya Waislamu. (ii) Waislamu watazikusanya tiketi za Wakristo, na Wakristo za Waislamu.

3. Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian kwa niaba ya Waislamu na Bwana Deputy Abdullah Atham Khan kwa niaba ya Wakristo watakuja kushindana.

4. Hakutakuwa na ruhusa ya mtu mwingine yeyote kuongea minghairi ya watu hawa wawili. Naam, hawa watu wanaweza kuwachagua watu watatu kama wasaidizi lakini hawatakuwa na ruhusa ya kuongea.

5. Upande wa upinzani utakuwa unaendelea kuandika ukumbusho sawasawa kwa lengo la kuuchapisha.

6. Hakuna mtu wa upande wowote atakayeweza kuongea zaidi ya saa moja.

7. Katika masuala ya kinidhamu uamuzi wa mwenyekiti

[13] Tafsiri kutoka kwa Kiingereza. (Mwenezi)

wa kikao ndio utakaokuwa wa mwisho.

8. Kutakuwa na wenyeviti wawili wa mkutano, yaani mmoja mmoja toka kila upande watakaochaguliwa wakati huo.

9. Kuteua sehemu ya kufanyikia mjadala litakuwa ni jukumu la Dr. Henry Martyn Clark.

10. Wakati wa mjadala utakuwa kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 5 asubuhi.

11. Wakati kamili wa mjadala utagawanywa katika zama mbili: Siku sita, yaani siku ya Jumatatu ya tarehe 22 Mei hadi 27 Mei. Na ndani ya wakati huo Bwana Mirza atakuwa na hiyari ya kutoa dai lake hili kwamba ukweli wa kila dini ni lazima uthibitishwe na ishara zilizo hai kama vile alivyodhihirisha ndani ya barua yake ya tarehe 4 Aprili 1893 aliyoiandika kwa Dr. Clark.

12. Halafu suali la pili litaibuliwa, kwanza itakuwa juu ya suala la uungu wa Yesu, na halafu Bwana Mirza atakuwa na hiyari ya kutoa suala lololote alipendalo lakini ndani ya siku sita.

13. Muhula wa pili pia utakuwa wa siku sita, yaani kuanzia tarehe 29 Mei hadi tarehe 3 Juni (kama kutakuwa na haja kiasi hiki). Katika kipindi hiki Bwana Abdullah Atham Khan atakuwa na hiyari ya kuyatoa maswali yake yafuatayo kwa kirefu:

(i) Huruma bila ya mbadala (ii) Kulazimisha na Kudra

(iii) Imani juu ya kulazimisha (iv) Uthibitisho wa Kurani kuwa ni Neno la Mungu (v) Uthibitisho wa jambo hili kwamba Muhammad[saw] ni Mtume wa Mungu. Yeye anaweza kuuliza maswali mengine pia kwa sharti ya kutozidi siku sita.

14. Tiketi lazima zitolewa hadi tarehe 15 Mei. Tiketi hizo zitakuwa za mfano kama ilivyoelezwa hapa chini.

15. Wakristo na Bwana Deputy Abdullah Atham Khan wamezikubali kanuni hizi kuwa ni zenye kuwajibika kutiiwa na wameyakubali maandishi haya kuwa ni sahihi:

“Kwa ushahidi, mimi (ambaye saini yake imetiwa hapa chini) kwa niaba ya Bwana Abdullah Atham Khan naweka saini, na kuhusu kuvunja sharti lolote kati ya masharti hayo yaliyotajwa hapo juu ni kwamba upande utakaovunja utahesabiwa kuwa umekiuka makubaliano”.

16. Wenyeviti na watoa hotuba watatia saini juu ya hotuba kwa ajili ya kuthibitisha usahihi wao.

Saini:
Henry Clark M.D. n.k. Amritsar, 24 Aprili 1893

**Mfano wa Tiketi**

Mjadala baina ya Bwana Deputy Abdullah Atham Khan wa Amritsar na Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.
Tiketi ya kuingilia kwa ajili ya upande wa Waislamu.
Muingize.............. Nambari.....
Saini ya Dr. Clark
Amritsar, 24.4.1893

**Mfano wa Tiketi**

Mjadala baina ya Bwana Deputy Abdullah Atham Khan wa Amritsar na Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.
Tiketi ya kuingilia kwa ajili ya Wakristo.
Muingize.............. Nambari.....
Saini ya Bwana Mirza

## Barua ya Rejista iliyotumwa mnamo tarehe 25 Aprili katika kuijibu barua ya Bwana Padri ya tarehe 24 Aprili

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [14]

Mheshimiwa, Mpendwa Bwana Padri, ukae salama.

Baada ya yaliyowajibika, nimeisikia barua yako toka mwanzo hadi mwisho. Mimi nayakubali masharti yote yaliyosainiwa tayari nawe na marafiki zangu na marafiki zako. Lakini kwanza kabisa jambo hili linatakiwa liwe wazi kabisa kwamba lengo la mjadala huu na mashindano haya ni lipi. Je utakuwa ni mjadala kama ile mijadala ya kawaida inayofanyika katika Panjab na India kwa miaka mingi baina ya Waislamu na Wakristo, ambayo matokeo yake ni kwamba Waislamu kwa rai yao wanakuwa na yakini kwamba katika kila jambo tumewashinda Wakristo, na Wakristo nao wanasema maneno haya wakiwa majumbani mwao kwamba Waislamu wameshindwa kujibu. Kama ndio iwe hivi, basi hiyo haina faida yoyote na ni kazi bure na hatima yake haionekani zaidi ya jambo hili kwamba baada ya siku

[14] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. (Mwenezi)

chache za kelele za mjadala halafu kila domo kaya apate fursa ya kubuni maneno ya kujithibitishia ushindi. Lakini mimi nataka kwamba haki ifunguke na dunia ipate kuona ukweli. Ikiwa kwa hakika Hadhrat Masihi[as] ndiye Mungu na yeye ndiye mola wa walimwengu na mwumba wa mbingu na ardhi, basi bila shaka sisi tu makafiri bali makafiri wakubwa kabisa, na bila shaka katika hali hii Islam haiko kwenye haki. Lakini kama Hadhrat Masih[as] ni mtu tu, nabii wa Mwenyezi Mungu na ana udhaifu wote wa kiumbe ndani mwake, basi hii ndiyo dhulma kubwa na kufuru kubwa ya Wakristo kwamba wanamfanya mja mmoja dhaifu kuwa mungu. Na katika hali hii hakuna dalili iliyo bora zaidi ya Kurani kuwa Neno la Mwenyezi Mungu kwamba imeistawisha tena Tauhid (umoja wa Mwenyezi Mungu) iliyokuwa imetoweka, na yale marekebisho yaliyokuwa yafanywe na kitabu cha kweli imeyafanya, na imekuja katika wakati ambapo ilikuwa inahitajika kuja kwake. Suala hili kwa hakika lilikuwa wazi kabisa kwamba Mungu ni nini na sifa zake zinatakiwa ziweje. Lakini kwa kuwa sasa Wakristo hawalifahamu jambo hili na mijadala ya kiakili na kimaandiko ya humu nchini India haiwapi faida yoyote, hivyo imekuwa ni lazima sasa mwundo wa mjadala ubadilishwe. Hivyo, kwa rai yangu hakuna njia iliyo mnasaba zaidi ya hii kwamba mashindano ya kiroho kwa njia ya Mubahala yafanyike. Nayo ni hivi kwamba

kwanza mjadala ufanyike kwa kila siku sita — mjadala ambao marafiki zangu wameshaukubali — na siku ya saba ufanyike Mubahala. Na pande mbili ziombe dua hii ndani ya Mubahala, kwa mfano (mshindani wa) kundi la Wakristo aseme hivi kwamba yule Isa Masihi Mnazareti ninayemwamini yeye ndiye mungu na Kurani ni uzushi wa mwanadamu, sio kitabu cha Mungu. Na kama mimi si mkweli katika jambo hili, basi ndani ya mwaka mmoja initeremkie adhabu ambapo kudhalilika kwangu kudhihirike. Na halikadhalika mimi nitaomba dua hii: "Ee Mungu Uliyekamilika na uliye Mtakatifu, mimi ninafahamu kwamba kwa hakika Isa Masihi wa Nazareti ni mja Wako na mtume Wako, si Mungu hata kidogo, na Kurani Tukufu ni Kitabu Chako Kitakatifu na Muhammad Mustwafa[saw]. ni mtume Wako kipenzi na mteule. Na kama mimi si mkweli katika jambo hili, basi ndani ya mwaka mmoja uniteremshie adhabu ambapo kudhalilika kwangu kudhihirike. Na, Ee Mungu kwa ajili ya kudhalilika kwangu jambo hili litatosha kwamba ndani ya mwaka mmoja isiweze kudhihirika toka kwako ishara ya kunisaidia ambapo wapinzani wote washindwe kupambana nayo. Na itawajibika kwamba kwa saini za pande zote mbili maandiko haya yachapishwe katika magazeti machache kwamba yule mtu atakayethibitika kufikwa na ghadhabu ya Mungu ndani ya mwaka mmoja, au kwamba katika kuusaidia upande mmoja zidhihirike

baadhi ya ishara za kimbingu ambazo zisiweze kudhihirika na kuthibitika katika kuusaidia upande wa pili. Hivyo katika hali kama hii, upande ulioshindwa ukubali dini ya upande ulioshinda au aitoe nusu ya mali yake yote kwa ajili ya kuisaidia dini ile kwa upande ulioshinda ambao ukweli wake umethibitika.

Mnyenyekevu,
Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian,
wilaya ya Gurdaspur